

*This document has been translated from Kiswahili using Google translate. The original Swahili document appears below.*

MINISTRY OF HEALTH, SOCIAL DEVELOPMENT, GENDER, ELDERLY AND CHILDREN

COVID-19 ASSESSMENT GUIDELINES FOR FOREIGNERS.

SECOND ISSUE, 04 JANUARY 2021

### **1.0 Introduction:**

The COVID-19 outbreak has continued to affect various countries since it was confirmed in December, 2019. As of 03 January 2021 a total of 83,322,449 patients and 1,831,412 deaths have been reported worldwide. Various countries have continued to take various measures, including the requirement to test the COVID-19 Infection for all travelers, to restrict international travel and to impose Lock down. Tanzania is one of the countries that has taken effective measures to control the transmission of COVID-19.

This guideline is based on the growing number of new patients reported daily in the world and the emergence of a new strain of COVID-19 (New Variant Strains) virus in some countries. At the same time, the increase in the cost of testing COVID-19 is due to the increase in travelers traveling abroad and tourists entering the country, technological changes in testing where some countries have requested increased IgM Antibody in tandem with PCR and increased demand for Sampling stations have introduced the revision of the Manual of the first edition of July 20, 2020. As a result, the Ministry has prepared a Manual to Test the Second Edition of the 4th of January 2021 for travelers traveling abroad and visitors to Tanzania including tourists.

### **1.1 Guide Areas:**

This guide sets out the procedure for applications, testing, how to get answers, border checks and testing costs for Travelers (all people traveling abroad from Tanzania including Drivers transporting goods and passengers to foreign countries, departing guests and Tourists).

### **1.2 Application and Testing Procedure:**

1.2.1 Traveler should be educated on how to get information from the Embassies over the need for a COVID-19 test

1.2.2 A traveler who needs a COVID-19 diagnostic service should arrive at the Regional Hospital or specialized facilities including all facilities that carry out daily surveillance of Influenza virus (Influenza Sentinel Sites) nationwide with proof of need for testing and with a passport. For Dar es Salaam Region, Muhimbili National Hospital, Amana Referral Hospitals, Mwananyamala and Tameke will be responsible for Sampling. Also Aga Khan Hospital, IST Clinic, Sinza Hospital, Mbagala Hospital and Kigamboni Hospital are also tasked with the exercise of taking samples and presenting them to the National Laboratory with the aim of reducing the congestion of customers waiting for the service at the National Laboratories during the testing exercise.

1.2.3 The Office of the Chief Medical Officer of each Region shall supervise this exercise of taking samples and sending them to the National Central Laboratory located in Mabibo, Dar es Salaam.

1.2.4 Traveler samples should be clearly identified by typing the words of the Region\_ITR name (International Traveler).

1.2.5 The traveler should be educated to test five days before the day of travel. The COVID-19 certificate will last for 14 days or will depend on the conditions of the country in which he or she travels.

**1.3 Procedure for obtaining answers and certification:**

Test results will be sent to the relevant Regional Medical Officer. For non-infected travelers they will be issued with certificates and their names will be sent electronically to the Characters and copies to the Regional Chief Physician and Border Health Officer at the border to facilitate verification and reduce inconvenience to Travelers and Drivers. Responses will be provided within 48 hours for Regions outside Dar es Salaam and 24 hours within Dar es Salaam Region before the trip.

**1.4 Border certification checks:**

Travelers who have COVID-19 certificates should be advised that their certificates will be verified at the borders (verification). This procedure can be done electronically.

**1.5 Testing costs:**

The cost of the COVID-19 tests will be USD.100 for any traveler traveling abroad including Tourists.

N.B: These payments should be made into the Government's Laboratory Laboratory Services account and the participants should be provided with Government electronic receipts.

This guide will be updated according to need.



**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**MWONGOZO WA UPIMAJI WA COVID-19 KWA WATU WANAOSAFIRI NJE YA NCHI.**

**TOLEO LA PILI, 04 JANUARI 2021**

**1.0 Utangulizi:**

Mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 umeendelea kuziathiri nchi mbalimbali toka ulipothibitika mwezi Disemba, 2019. Hadi kufikia tarehe 03 Januari 2021 jumla ya Wagonjwa **83,322,449** na Vifo **1,831,412** vimeripotiwa Duniani kote. Nchi mbalimbali zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo sharti la upimaji wa Maambukizi ya COVID-19 kwa wasafiri wote, kuzuia safari za Kimataifa na katazo la kutoka nje (Lock down). Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimechukua hatua madhubuti na kudhibiti maambukizi ya COVID-19.

Mwongozo huu unatokana na kuongezeka wagonjwa wapya wanaoripotiwa kila siku duniani na kuibuka kwa aina mpya ya vimelea vya Ugonjwa wa COVID-19 (New Variant Strains) katika baadhi ya nchi. Sambamba na hilo, kupanda kwa gharama za upimaji wa COVID-19 kunakochangiwa na ongezeko la wasafiri wanaokwenda nje ya nchi na Watalii wanaoingia nchini, mabadiliko ya teknolojia katika upimaji ambapo baadhi ya nchi wameomba kuongezeka kipimo cha **IgM** Antibody sanjari na **PCR** na kuongezeka kwa mahitaji ya vituo vya kuchukulia Sampuli imepelekea maboresho ya Mwongozo toleo la kwanza la tarehe 20 Julai, 2020. Kutokana na hali hiyo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Upimaji **Toleo la Pili la tarehe 4 Januari 2021** kwa wasafiri wanaokwenda nje ya nchi na wageni wanaotembelea Tanzania wakiwemo Watalii.

**1.1 Maeneo ya Mwongozo:**

Mwongozo huu unaweka utaratibu wa maombi, upimaji, namna ya kupata majibu, uhakiki mipakani na gharama za upimaji kwa Wasafiri(watu wote wanaokwenda nje ya nchi kutokea Tanzania wakiwemo Madereva wanaosafirisha mizigo na abiria kwenda nje ya nchi, wageni wanaoondoka na Watalii).

**1.2 Utaratibu wa Maombi na Upimaji:**

1.2.1 Msafiri aelimishwe kupata taarifa kutoka katika Ofisi za Ubalizi wa nchi anayotaka kwenda juu ya uhitaji wa kupimwa ugonjwa wa COVID-19.

1.2.2 Msafiri atakayehitaji huduma ya upimaji ugonjwa wa COVID-19 afike katika Hospitali ya Mkoa au vituo maalumu vilivyo dhinishwa ikiwemo vituo vyote

vinavyofanya ufuatiliaji wa kila siku wa vimelea vya Influenza (Influenza Sentinel Sites) nchini kote akiwa na uthibitisho wa uhitaji wa kupima kwa nchi anayotaka kwenda ikiwemo hati ya kusafiria. Kwa Mkoa wa Dar es salaam Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa Mkoa Amana, Mwananyamala na Temeke zitahusika kuchukua Sampuli. Pia Hospitali ya Agakhan, Kliniki ya IST, Hospitali ya Sinza, Hospitali ya Mbagala na Hospitali ya Kigamboni pia zitahusika na zoezi la uchukuaji sampuli na kuziwasilisha Maabara ya Taifa kwa lengo la kupunguza msongamano wa wateja wanaosubiri huduma hiyo Maabara ya Taifa ili kwa kiasi kikubwa Maabara ibaki na zoezi la upimaji.

- 1.2.3 Ofisi ya Mganga Mkuu kila Mkoa isimamie zoezi hili la uchukuaji wa sampuli za na kuzituma katika Maabara Kuu ya Taifa iliyoko Mabibo, Dar es salaam.
- 1.2.4 Sampuli za wasafiri ziainishwe vizuri kwa kuandika maneno ya jina la Mkoa\_ITR (International Traveller).
- 1.2.5 Msafiri aelimishwe kupima siku tano kabla ya siku ya kusafiri. Cheti cha COVID-19 kitadumu kwa muda wa siku 14 au itategemea masharti ya nchi husika anapokwenda.

### **1.3 Utaratibu wa kupata majibu na kupewa vyeti:**

Majibu ya vipimo yatatumwa kwa Mganga Mkuu wa Mkoa husika. Kwa wasafiri ambao hawatakuwa na maambukizi watapewa vyeti na majina yao yatatumwa kwa njia ya kielektroniki kwa Wahusika na nakala kwa Mganga Mkuu wa Mkoa na Afisa Afya walioko mipakani kurahisisha uhakiki na kupunguza usumbufu kwa Wasafiri na Madereva. Majibu yatatolewa ndani ya saa 48 kwa Mikoa nje ya Dar es salaam na saa 24 ndani ya Mkoa wa Dar es salaam kabla ya safari.

### **1.4 Uchunguzi/ uhakiki wa vyeti mipakani:**

Wasafiri ambao wanavyeti vya COVID-19 washauriwe kuwa vyeti vyao vitahakikiwa mipakani (verification). Utaratibu huu unaweza kufanyika kwa njia ya kielekitroniki.

### **1.5 Gharama za upimaji:**

Gharama za vipimo vya COVID-19 zitakuwa ni **USD.100** kwa msafiri yeyote anayesafiri kwenda nje ya nchi ikiwemo **Watalii**.

**N.B: Malipo haya yalipwe katika akaunti ya Serikali ya Huduma za Maabara ya Taifa na wahusika wapewe stakabadhi za kielekroniki za Serikali.**

Mwongozo huu utaboreshwa kulingana na mahitaji.

Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**